REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Thursday, 12th November, 2020

The House met at the Assembly Chambers at 9.00 a.m.

[The Deputy Speaker (Hon. Daniel Nyausi) in the Chair]

PRAYERS

Deputy Speaker: What is it Hon. Stephen?

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you, Mr. Speaker. Today is a very bad day for this Assembly because yesterday we had a very hot debate in this Assembly and by the end of it there is what we had agreed on. Mr. Speaker, we complained to you that there was a motion that was to be drafted by yesterday and you said that you would follow it to the letter to see to it that our motion will be in today's order paper but what we can see today is that you are misleading the House and you are also being driven by some powerful individuals to drive this House like a private entity.

There is a motion that is here and we brought it in the morning to the clerk of the Assembly and you assured us that we are going to get it but we haven't. We must be told in clarity what is happening and if you yourself cannot drive the Assembly you should also get out of that seat. You were elected by people from Mukogodo East to come here and make things right for them but it seems that you have joined hands to bring us down.

Mr. Speaker, we are also going to demand that the Mace also be taken from its place even if it is going to take a fight today. If you are being used, today is Mutuiri's day and the others to follow. We were elected to represent people in this Assembly and we are going to do so without being intimidated. Thank you.

Hon. Mutahi Muritu: Mheshimiwa Spika, nasimama kupitia kiti chako. Spika wa Bunge kutumia busara zake akiona hali ya Bunge analoliendesha ama kuna makubaliano fulani kutoka kwa vikao za nje au ndani, akiona ya kwamba hali sio nzuri, anafaa kutumia busara. Mheshimiwa Spika, nakuomba ya kwamba kwa miaka mitatu ambayo tumekuwa hapa katika hili Bunge isiwe siku ya leo itaingia kwenye kumbu kumbu kwamba wewe ulipokuwa umekalia hicho kiti tukufu, watu zaidi ya laki tano katika Laikipia wanakuangalia.

Sasa hivi tunataka kujadili na kila kitu kimepangwa na wewe ukiwa kwenye hicho kiti nakuomba na pia naomba Wajumbe ya kwamba kama utatumia busara zako uone ya kwamba hii kitu haiendi kwa utaratibu, tafadhali usije ukairuhusu kwenye hili Bunge kwa sababu tutatumia nguvu na hilo sio hoja na sisi ni Waheshimiwa Wajumbe. Kama kuna mswada ambao ulikuwa unafaa kuwa umewasilishwa tafadhali tutumieni busara sisi wote na twende kwa utaratibu. Uende katika Kanuni namba moja, kama hali ya hewa sio nzuri katika Bunge lolote, unastahili kutumia hilo kanuni.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mheshimiwa Spika, hatutaki kuleta mambo ya ajabu kwa sababu sisi ni Wajumbe na kama safari imeanza, hakuna haja ya kuzuia. Kuhusu *order paper,* katika kanuni zetu zinasema ya kwamba niwe nimepewa masaa ishirini na manne. Sasa hii *order paper* inaletwa hapa sasa hivi. Kwani tunatumia nguvu? Hatutumii nguvu bali kile kitu ambacho kinafaa kufanyika hapa tunafaa kutumia busara. Kama hatuelewani sasa tunakuja kufanya nini hapa. Lazima kuwe na vikao na kama kuna kitu kinatakikana lazima kiwepo.

Mheshimiwa Spika, wewe ndiye unafaa kutoa taarifa na haujatoa ilhali ulikuwa kwa kikao cha asubuhi. Tumezoea na tumewakubalia na hata sasa unaona ya kwamba kama hii imeletwa na kuwekelewa juu ya meza. Kweli hiyo ni kazi? Tunaweza toa vurugu lakini hatutaki kuenda kwa mwenendo huo. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika, ninakusihi kwa heshima yako, kama Naibu wa Spika usitumike visivyo kwa sababu hao hautawaweza kulingana na vile hali ya hewa ilivyo.

Mimi ni naibu wa Kiongozi wa Walio Wengi katika Bunge hili na kwa hivyo hata ninapoongea ninaongea ninachokijua mwenyewe hata kama jana sikuweko. Kwa hivyo tutumieni busara tusije tukaleta vitu zingine ambazo hazitaleta tija katika Bunge letu. Kama ni utaratibu utumike na kama ni vikao vya nje na vya ndani tuendelee kwa sababu kinachoendelea hapa ni maslahi ya wananchi wa Laikipia.

Kwa hivyo tujiangalie sana kwa sababu hatutaki sarakasi lakini sisi katika utamaduni wetu husema ya kwamba mama akishapata mimba na ionekane haiwezi fichwa tena. Tukubaliane hapa ya kwamba hali ya hewa ya Bunge la Kaunti la Laikipia siku ya leo sio nzuri. Kwa hivyo tusiende kusema ya kwamba tunabeza tu yaliyoko Bunge hili. Leo asubuhi tangu tuingie Bunge hili hatujawahi kuangaliwa kama tuna bunduki lakini naomba kwa heshima na busara tusianze kudharauliana au kutumia nguvu kwa sababu hatutaweza hayo.

Tena ni kwa nini tunataka kuleta mambo ya ajabu. Kama kuna kitu ambacho kinaendelea katika hili Bunge basi wacha tufuate utaratibu kwa sababu hili ni Bunge la heshima na hadhi. Kwa hivyo mimi nakusihi Bwana Spika kwa sababu tunakaa jopo la Spika nawe na kulingana na yale mafunzo ambayo tunayopata, hawa watu huwa twawaongoza lakini kama hawataki tuwaongoze kwa utaratibu huo, huoni kama kwamba hata sisi katika jopo letu la Spika tunakiuka kanuni?

Huu sio ukumbi wa densi bali hili ni Bunge tukufu. Wewe ni Naibu wa Spika na uko katika jopo la Spika na tuko na wanachama walioko kwenye jopo la Spika na kwa hivyo tumieni utaratibu unaostahili kuleta amani. Kwa hayo mengi au machache ninamshukuru Mwenyezi Mungu. Kanuni zetu zinatuambia kwamba kama tunapinga tuko sawa, ukisema mmoja wasimame watano, tutaendesha nani? Tutasimama na tutapinga kwa sababu tunaruhusiwa na Kanuni zetu za Bunge.

Kwa hivyo tumia busara Mheshimiwa Spika ili tuweze kuenda kwa utaratibu. Wewe sio Spika, kwa hivyo usije ukasahau ati wewe sio Spika na kinachojadiliwa, Spika ndiye mwenyekiti lakini wewe umewekwa kama kivuli. Nakuomba kakangu na ninakuheshimu lakini usije ukatumika vibaya. Kinachojadiliwa ulikuweko jana nami sikuweko na ukiona tukipinga ni kwa maslahi ambayo yako katika kanuni zetu.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Sisi tumekuwa wastaarabu lakini husemekana ya kwamba diplomasia ikishindikana tunatumia nguvu lakini hatutaki hivyo. Ninaamini ya kwamba wewe una uwezo kwa hivyo tumia diplomasia badala ya nguvu. Asante.

Hon. Chris Mark: Thank you, Mr. Speaker. I want to say that there is a reason why this Assembly has got two doors. One on that side and another on this side and it is wrong that this door was closed because of safety. If there is a fire in this House or commotion, all of us cannot fit through one door. As much as the temperatures might be high, let that door remain open. I think I told you that but I think that you did not communicate.

Mr. Speaker, the other issue here is that yesterday we told you our grievances and you refused to give us directions saying that words cannot be put in the mouth. We are not silly or stupid because we knew what you meant. A Member of staff could not even draft a motion because he ran off at a very high speed. I even said in this House that we do not blame that staff but you told us that there is a procedure and even the Hon. Minority said that if it could be brought to them in the HBC, we would have it.

That motion was ready by yesterday meeting even when phone calls of staff here were switched off. Everybody in the table clerk's office disappeared. Even the Clerk Assistants disappeared because they were afraid. So the gravity of the matter is that let no person seat here thinking that the office are intertwined. That office will be there beyond that person. So let the directions which are given by the Members here be respected because we directed for that motion to come.

You said that we need time and even the Minority said here that there is usually a procedure. This morning we are looking at this paper and we cannot see our motion. We are not going to lie to you Mr. Speaker. You are being reminded that you are the Deputy Speaker and I reminded you yesterday that you wear two hats. One for MCA and the other one for the Speaker and that should be able to help you balance and know that at times you are supposed to see the grievances that are here. At night from yesterday to today phone calls have been made to staff which we have the recordings and even to these Hon. Members, text messages and even incentives which we have the evidence that don't do this because you will get this.

I am even wondering why it is becoming difficult because you are even making our work easier. If that motion is taking time to come here, what is being hidden that the motion is delaying. When we say that someone should be suspended, we are not saying that he should be fired but we are just saying that they go ahead. Why is so difficult for that person…

Deputy Speaker: Hon. Members, let me please remind you that we are in the House and if you opt to clap please use the procedural way when we are in the chambers. Hon. Ndiritu let us respect the House.

Hon. Chris Mark: Mr. Speaker, you are calling this an Honourable House and even the National Assembly was an honourable House when the Speaker Justin Muturi was poured water. It was still an honourable House when the former Senator of Machakos, Hon. Muthama had his trousers torn in the Speaker's gallery. It is always an Honourable House but if diplomacy and democracy fails like the Hon. Member said then we use the thorax but we don't

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

want to go there. My humble request so that we do not go back in circles is that we adjourn this sitting and let this paper be amended because need a way forward. That motion was drafted 24 hours before the time.

Mr. Speaker, I know that that office and that seat which you are sitting on has got a lot of pressure. I can even see that you are not sitting on it comfortably today and I understand. You might even be a victim of these phone calls because they have been many. Let that motion come and if it falls let it fall because that is what democracy means. It cannot be dictatorship that it won't come at all costs. In fact, I have heard people say that let us delay this motion till Tuesday and let us have more time to lobby Members and give incentives. Some Members here who are on a rent seeking mission that a weekend cannot end without them getting Kshs.20, 000, 50,000 or a 100,000. Here Members are rich and I believe so.

Members don't want Kshs. 50,000 or a 100,000. I am just saying that because if there is somebody who is thinking that by delaying this motion and giving Members some money will help, we cannot be bought. For example, look at the suit that Hon. Meshami is wearing, it is almost 30,000. Look at the suit that Hon. Matunge and Hon. Kiguru who has just walking are wearing, they are very expensive suits.

So if there are people who thinks that by delaying this motion you will make phone calls and intimidate, they are lying to themselves because that motion must be there today. It is the Speaker who said that if we do our part then the House will deliver. Yesterday these offices were vacant and I think that I only saw the Serjeant at Arms here and there to the point where you would get to an office and find papers flying in the air. It is like the people were taking off.

I want to assure the members of staff that this is an institution but not a personalised item. They should not fear but just do their role. Thank you, Mr. Speaker, let us adjourn this sitting and let the order paper be amended so that we go ahead with the matters of the House.

Hon. Robert Maina: Asante, Mheshimiwa Spika. Nashukuru Wajumbe na mimi ndiye nilikuwa Bunge siku ya leo hata kama kuna biashara nyingine mbele yetu. Mimi nilikuwa hapa saa moja asubuhi nikileta ule mswada kwa njia ambayo inafaa kulingana na vile mlitueleza jana. Ingawa hata naibu wa karani alitoroka na akazima simu, huo mswada ulikuwa imekamilika kulingana na vile mlikuwa mmetuambia.

Ningeteka kutoa uwoga kutoka kwa wafanyikazi wa hili Bunge na wajue ya kwamba tunajua ya kwamba wamekuwa wamekaliwa miaka nenda miaka rudi. Mimi nina uhakika ya kwamba hao huwa wanapiga magoti asubuhi, saa saba na jioni kwa yale masaibu ambayo huwa wanapitia, Mungu wa wafanyikazi ako uhai na tena ni yule Mungu wa Yakubu na amesikia maombi yao. Liwe liwalo aidha mukose *quorum* HBC au hao Wajumbe wapigiwe simu zenye tumeona wakipigiwa ili wahongwe, Bunge la Laikipia litasimama hadi mswada wangu wa kusimamisha karani uwe kwa hili meza. Mimi ndiye mwenye kuuleta pamoja na hawa Wajumbe.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Sileti kama Robert lakini tunauleta tukiwa kama Wajumbe na wale ambao watakaa kando na huu mswada bado tutawaona. Tunajua ya kwamba hapa tuko na MCA wakuu na tulisema jana ambao huwa wanapata mshahara maradufu ili waweze kusitisha Bunge…

Deputy Speaker: Just a minute Hon. Robert. You are being interrupted because of the noise of other Hon. Members who have been given their chance to deliberate and we are not going to continue like this because it is not right. With all that noise that person will not even hear you. Let us give the Member an ample time to finish what he intends to say.

Hon. Robert Maina: Asante, Mheshimiwa Spika. Ni vizuri ujue ya kwamba hawa Wajumbe hawana shida. Kama haujawaona waking'oa hizi viti kwa sababu tutazing'oa, mambo bado. Hizi viti tutang'oa na hakuna haja nikufiche. Kama pesa ya wana Laikipia inapotea katika hili Bunge na hizi viti zimejengwa na pesa za wana Laikipia, kwa nini tusizing'oe ili tusikizwe.

Jana nilisema ya kwamba siongei kama Robert lakini kama Mjumbe wa Ngobit ambaye alichaguliwa na watu Zaidi ya elfu kumi na nilikuja hapa kuwasimamia. Kama ule mswada ambao mimi mwenyewe nimeleta kupitia hawa Wajumbe hauko hapa kwa meza yangu, Mheshimiwa Spika fanya hima, ahirisha Bunge kwa muda wa dakika thelathini au lisali moja ili nyinyi muweze kuketi kwa sababu wale ambao wanaketi katika HBC hawako mbali. Wengine tulikuwa tunawapigia wanasema ya kwamba wanakuja ilhali tunajua ya kwamba walipigiwa simu na kuambiwa wasije lakini hiyo haina shida. Hata kama ni usiku, kesho, kesho kutwa, mtondo na mtondogoo bado tutakuwa hapa.

Bwana Spika, fanya hima. Wana Laikipia wanangojea ripoti ya leo na hata jana ilipeperushwa katika mitandao. Kenya nzima wanangoja kujua Bunge la Laikipia liko kwa hali ipi kwa sababu kuna bishara ambazo zimesimama upande wa Executive. Ni kwa nini mnataka kusimamisha Bunge? Kwani hili Bunge limekuwa la familia? Bwana Spika, uko na nguvu hata kama wewe ni naibu wa Spika. Kwa sasa umeketi kwa hicho kiti kumaanisha ya kwamba wewe ni Spika. Kwa hivyo amua, itisha dakika thelathini au lisali moja ili niweze kupata mswada wangu hapa ili tuweze kuendelea. Asante.

Hon. Irene Wachuka: Asante sana, Bwana Spika kwa kunipatia hii nafasi. Kuna mambo ambayo mtu akisimama hata anashindwa ni aseme nini. Jana tuliongea kama Wajumbe wa hili Bunge na tukasema ya kwamba tungetaka tuwe kitu kimoja. Mheshimiwa Jacob akasema ya kwamba kama kitu kimeletwa, wewe unakalia kiti cha Spika ukiwa naibu wa Spika na wewe ndiye ambaye tunaletea shida zetu. Uko na kofia mbili na umetoka kiti cha MCA na tukakupatia mamlaka ya kuwa naibu wa Spika kwa sababu zote hatungetoshea kwa hicho kiti lakini sasa yale ambayo umetuonyesha na sio mara ya kwanza…

Deputy Speaker: Order Hon. Zamzam! Members, let us give each other time and let us not turn these things into other businesses. This is a House of order therefore talk in order and clap the way you are supposed to clap. Everybody will be given their time to deliberate but once we start making unnecessary movements them we are not moving in the right direction.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Irene Wachuka: Bwana Spika, jana tulikuwa na kikao hapa na wewe na tukasikizana. Sasa kuingia hapa zile karatasi tunazoziona ni hizi tumeletewa. Sijui tuseme nini inaendelea. Sina shida na wafanyakazi kwa sababu wako chini ya mtu mwingine ambaye ni Spika na Katibu wa Bunge. Askari ninawaona wameletwa wengi na sio wale huwa hapa. Sijui walikuja kufanya nini ama wameletwa kufanya nini. Tuko na askari wetu wa Bunge na tangu tuingie hapa Bungeni hatujawahi kuchunguzwa na askari. Kwani jana kulifanyika nini? Ninataka kusema hivi, Bwana Mutuiri ambaye ni Karani wa Bunge hili na Mheshimiwa Waigwa ambaye ni Spika wajue kunayo serikali ya Uhuru Muigai Kenyatta. Hatutasimama hapa tusumbuliwe na Spika na Katibu wa Bunge.

Tulikuwa tuketi chini na ukiona nyumba yako inaharibika unamwita mke na watoto wako mkae chini mnong'onezane mjue ni wapi shida iko. Watu wanatatua matatizo yao ila sisi hatukuitwa. Tunajaribu kumwita Spika anapiga simu na usiku simu ndizo hizi tukiulizwa na kila mtu kule tuliko. Wengine wanatumiwa kuwaita watu. Sisi hatutaki pesa wala kuitwa. Tumekata kauli kulainisha hili Bunge na tutailainisha. Wafanyakazi hapa wanakaa kama watu wa Rwanda sio kama wako Kenya. Ukimuita mfanyakazi anakimbia mbio asionekane akisimama na wewe. Kwani hapa ni Rwanda? Uhuru waja leo wala sio kesho, na tumeamua uhuru waja. Tunataka kila mtu apate haki yake, Mheshimiwa na wafanyakazi.

Hatulaumu kama vile Mheshimiwa amesema. Nikiwa nimeajiriwa na mkubwa wangu amesema nitatoroka. Hata yule Kosgei alitoroka sikumbeba kwa sababu akija kuonekana amefanya hicho kitu kesho hatakuwa kazi na sio vizuri afutwe. Tunataka kusema hata yeye Karani wa Bunge anaweza kufutwa. Si ataenda hata yeye? Ama aende Bunge lingine. Kunayo serikali na ujue iko na masikio inasikia. Haya maneno yaliyokuwa hapa jana yanajulikana Kenya nzima na sisi tungetaka Spika ajitokeze mahali amejificha akiwa na katibu wa Bunge. Tunajua wako hapa na wanatuma majasusi wao. Wapigiwe simu waambiwe kesho na kesho kutwa na nitaongea kwa Kikuyu. Tutakaa hapa hata kama ni siku tatu tukiwasubiri. Lazima hili Bunge lisimame vile linatakiwa. Hakuna kurudi nyuma, na hatutapigana kama wajumbe. Kupigana kwetu ni kuona haki imetiiwa.

Deputy Speaker: What is it Hon Nyawira?

Hon. Catherine Nyawira: Mr. Speaker, I am speaking on a point of order because I think the language the Hon. Member is using is unacceptable before this House because this is not a market place.

Deputy Speaker: Hon. Irene John, I think you were using part of Kikuyu or French but I think it was just a saying you were not conversing on the same so it is fine.

Hon. Irene Wachuka: Asante sana, Bwana Spika kwa kunikinga. Ninataka kusema hivi, mimi sina vita na mfanyakazi yeyote…

Deputy Speaker: What is it Hon. Stephen?

Hon. Stephen Ndiritu: Bwana Spika, nilikuwa ninataka ufafanuzi zaidi kwa Mheshimiwa Nyawira atueleze kama yeye ndiye amekuwa kiongozi wa Bunge kujua ile lugha inatumika. Inaweza kuwa yeye ni mmoja wa wale ambao wanajaribu kutukandamiza ama wamelala usiku wakihongwa ndipo ninauliza kwa sababu tunawajua…

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Deputy Speaker: Hon. Ndiritu that is enough for asking that clarification but let me say that as much as people think we have some super Members of County Assembly, I have no idea and I do not think we have such. Hon. Nyawira has a right as a Member of this House for such clarification because Hon. Irene John did not specify that she is using a saying or something. I do not really see any reason as to why we try to crucify the Hon. Member because she just said it is for clarification. It is not even the Member who gave it but I and the Member are satisfied, so let us go ahead. Hon. John Irene, are you done?

Hon. Irene Wachuka: Asante, Bwana Spika. Ili niketi ndipo mwingine aongee kile kitu ningetaka wewe ukiwa umekikalia kiti ni utupe japo lisali moja ama dakika thelathini mswada wa Mheshimiwa Roberto ufike. Sio wake ni wetu sote kwa sababu kila kitu kiko sambamba na tayari na maneno hayo yaishe. Kama haitaletwa sijui nini itaendelea. Ningeuliza kwa vile tunajua Spika na Katibu wa Bunge wako karibu hakuna vita ila watu waketi ili tujue njia ya kuendelea. Kama watu waliajiriwa na tumesema hata kama wako na barua hakuna kuendelea. Juzi na jana tuliongea hapa, na nitarudia, *wage bill* ya hili Bunge ilisemekana iko juu. Kama *wage bill* iko juu, watu wengine waliajiriwa kwa nini? Wale wako hapa kwa nini hawakupandishwa ngazi? Kuna wengine pengine waliajiriwa wakati wa mabaraza ya miji na kwa kile kiwango chao wanaweza kupewa cheo kimoja tu na siku zao ziishe.

Kile ningetaka kusema tafadhali tukiwa katika hii nyumba ya heshima tunaonekana eti tunazungushwa hivi. Ati leo ni Ijumaa hiki kitu kiwekwe Jumanne ili watu wengine waongeleshwe. Mimi sitaki kuongeleshwa na mtu. Nimeamua na hakuna mtu aliniambia niamue, nimeamua kusimama na Wanjiku aliye mashinani na kwa hivyo mimi…

Deputy Speaker: What is it, Hon. Matunge?

Hon. Peter Matunge: Mr. Speaker…

Deputy Speaker: On what point are you rising, Hon. Matunge?

Hon. Peter Matunge: Mr. Speaker, you need to listen to what I want to say…

Deputy Speaker: Hon. Matunge, I cannot listen to what you say. Order, Hon Matunge! Serjeant-at-arms, Hon Matunge, we cannot run this House that way. Hon. Irene John was on the floor; she was not yet done. Once I see your microphone on I suppose you were standing on a point of clarification or order and that is how we should. I will give you your time to say what you want to but at the right time please. Let us Hon Members respect the House.

Hon. Irene Wachuka: Nimemaliza Mheshimiwa Spika

Hon. Salma Zamzam: Asante sana, Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi pia niungane na wenzangu. Kama vile jana tuliweza kusema hakuna mjadala ama chochote kitaendelea hapa Bungeni na ningewaomba Wabunge wenzangu waweze kunisikiza. Hakuna kitu tuliweza kufanya jana bali tulisimamisha Bunge ili tupate kilio na haki ya watu zaidi ya laki tano wa Laikipia. Ukiwa kwenye hicho kiti ninasikia wewe ni Naibu wa Spika ila sasa hivi wewe ni Spika na umekikalia kidete. Usitingishwe na mtu. Jana Waheshimiwa walilia na wakaomba haki mswada uingie kwa Bunge kwa sababu ya kukiukwa kwa sheria kwa kuajiriwa kwa wafanyakazi hapa Bungeni. Kunao wale waliokandamizwa hata vyeo hawajapandishwa.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Ninasimama kama Zamzam na sitatishwa wala kubabaishwa. Ninasimama kama mfugaji aliyetumwa na serikali ya Jubilee kuwawakilisha wafugaji. Sina wadi ila ninasimamia kaunti nzima. Ni aibu sana nikiwakilisha wafugaji lakini wakija kuajiriwa ni kama madereva na kazi duni kisha tunaambiwa tumepewa wafugaji wanne. Pia wetu wamesoma na wako na shahada hata kama inasemekana kusoma sio suruali. Wako na suruali na wamesoma hao vijana na wasichana wetu. Nitasimama na nipige kelele mnipende ama munidharau, mniongee na kunitishia sitarudi nyuma hadi kifo kuwatetea wanyonge katika kaunti hii na wafugaji waliokandamizwa. Hata kupandishwa vyeo kwenyewe wanakosa.

Ukiwa kwenye hicho kiti wewe ni Mwakilishi wa watu wa Mukogodo mashariki lakini tunafaa kuongea ukweli na haki. Kunaye msichana alikuwa apandishwe cheo ila alienda Samburu kwa sababu alikosa kwa sababu ya ukabila. Sitaogopa, nitarudia kwa huo mwaka mmoja na miezi iliyosalia kusema hivyo. Sikuletwa hapa kama *flowergirl* na wafugaji. Nikitoka hapa nje nitaongea vivyo hivyo ili wafugaji wote wasikie Kenya nzima na haswa Kaunti ya Laikipia nzima.

Ninashukuru upande wa Gavana Ndiritu Muriithi anaangalia hadi jamii na kabila lakini hapa tukiangalia kunayo kabila na dini haziko. Dini ya Kiislamu ni Chris Mark na mimi katika Kaunti hii. Hatuwezi kupewa kipao mbele na siogopi kusema. Huwezi kunitishia, hukunileta hapa wala sikuletwa na baba ama mama ya mtu hapa. Wacha iwe mbaya na iwe hivyo na tutaendelea hivyo. Niko na uchungu sana Mheshimiwa Spika. Sasa hivi tungefaa kuangazia ajenda nne za Rais Uhuru Muigai Kenyatta na tumsikize akiongea lakini kwa sababu ya wizi na matajiri, maskini hawawezi kupata kazi katika Kaunti ya Laikipia. Kunao watoto ambao wazazi wao wanauza *chang'aa* na kuchoma makaa kwa sababu hawana kucha ndefu. Ninasimama hapa nikijiita *super MCA*. Siwezi kuwasaliti watu wa Laikipia na wafugaji. Ninawaomba wafugaji mnisikie n kunishikilia hata nikitishiwa, sitaogopa.

Ninaomba usinipigie simu ukiwa kiongozi uanze kuniambia maneno. Hua inasemwa mwacha mila ni mtumwa. Leo niko pale kwenye ile mila. Tunasema watakesha kisimani lakini tutazidi kuyateka maji. Tutayateka tukibaki wafugaji watatu ama wawili na tutasimama. Wacha tusimame na ndugu yangu Mheshimiwa Matunge hata tukiambiwa hivi na vile. Mheshimiwa Matunge tusirudi nyuma wala kubanduka. Tunasema kama hamwezi kukaza kamba hivyo viti tutavikalia ili tusikize huo uzito wa wajumbe waliochaguliwa.

Kina mama mlio hapa, Waheshimiwa Nyawira, Kibue na Wachuka, wacha tukaze kamba tutetee haki za kina mama. Tunaona kina mama ndio wanaweza kutetea haki za Laikipia. Sina ndugu wala dada niliyemleta, ninataka kuhitimu. Kunao wale hapa tunawajua hawajaajiriwa, tunaomba waajiriwe kwa sababu wameomba kuajiriwa wanaambiwa hawawezi. Tunajua kila kitu nje na ndani na kama uko na swali nitafute nje na ninakuomba usinipigie simu kwa sababu utajipata pabaya. Ninaomba hayo na nitasimama na wenzangu tupe lisali moja.

Ninamshukuru Mheshimiwa Veronica na Mheshimiwa Jacob pia. Hiyo ni kamati inayoweza kutengeza sheria. Wabunge tuwache kuwarudishia lawama wafanyakazi. Wanafuata kile wanaambiwa. Hata wewe ukiwa mke wa mtu unafuata kile mumeo anasema. Unajua Waswahili wanasema ukweli yauma. Hao wakikukagua tafadhali kubali wafanye kazi.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Makatibu wakifanya hivi kubali wafanye kazi lakini inasemwa siku ya arubaini ikifika imefika. Ukiona vile tunazungushwa mchezo wa paka na panya kuna kitu kimefichwa.

Tafadhali kama ulikubali kuingia kwa kikundi ama hilo kanisa letu usitoke kwa sababu ya vitisho ama kwa sababu tunasikia Jumanne kutakuwa na nini. Wacha hiyo Jumanne tutetee ukweli na haki. Letu ni kusema irudiwe nyingine ya haki na ukweli na hakuna kitu kingine. Ninasema hiyo Jumanne isifike, wacha mnipe nafasi turudie. Hiki kitu kirudiwe upya na Katibu wa Bunge aambiwe. Ninasikia Spika yuko humu, tafadhali kuja. Tulikupa kura zaidi ya ishirini, njoo usikize kilio cha waheshimiwa wanaotaka ukweli na haki, na *Super MCA* ambaye amesimama na wana Laikipia na wanyonge katika hii kaunti.

Hatuwatetei wale ambao hawajaajiriwa tu ila wafanyakazi walio katika Kaunti hii wanaonyoshewa kidole cha lawama na kukandamizwa. Sina mengi ila ninaungana na wenzangu mia kwa mia kutetea haki za wana Laikipia haswa wafugaji. Lazima tupate hizo haki na lazima wapandishwe vyeo. Sio mahali wafugaji wako wanazuia kupandisha watu vyeo. Tunajua, msituone hapo, ujasusi unafanya kazi. Mungu awabariki na wale tunaowatetea wanyonge tuendelee vivyo hivyo mpaka tumalize mkondo. Wale hawako na sisi Mungu awabariki pia kila mahali kunakuwa na vyama tofauti. Tuko pamoja na nyinyi kama wabunge kwa kila kitu lakini wacha tuogelee kwa mirengo tofauti. Wacha twende hadi tugonge mwamba na tukishindwa ama tukiendelea ni sawa. Mungu awabariki.

Hon. Peter Matunge: Hon. Member, the Speaker has given me a chance so you just have…

Deputy Speaker: It is true but when you were away, I gave Hon. Matunge

Hon. Peter Matunge: Mr. Speaker, I first wish to say this. These Members, the security team are here to provide us security but not be used to threaten us. One thing I just want to say before what I wanted to is that in every county the head of security sits in management meetings but in this county of Laikipia they are not anywhere in all those issues of management. I am saying this that we have talked a lot and yesterday we discussed a lot. I do not see the need for us to continue repeating and talking. I have a lot to say on this issue because you said yesterday it is your right. We told you to give a directive and you said it is your right. We were not stupid as the Hon. Member has said. We knew what we were saying but you insisted on the same. We went to the office of the Deputy Clerk and he disappeared and switched off his phone. The people who were supposed to draft the motion disappeared and switched off their phones.

We took our own efforts and drafted the motion and by six, the motion was ready. It is here, there is the notice of motion and the motion itself. We tasked you to convene a HBC meeting and it is this House which constituted HBC. If they fail to do their work then we do another HBC. This issue of making the County Assembly of Laikipia a private property should end today. We know the leadership, the Speaker and the Clerk, is around. They are misusing you and you should avoid being misused.

You are the elected Member of County Assembly for Mukogodo East. If today we remove you as the Deputy Speaker you are still a Member of this House. There are people who if we remove they will not be Members of this House. We said, and I want to say this is what

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Members agree, that there is no business that will continue until this motion is factored in the order paper. We do not want to talk more on that. We have to stop this until a supplementary order paper has been supplied to us and we have this motion in the paper. If it is not that there is nothing that will continue in this Assembly.

Hon. Jacob Endom: Asante sana, Bwana Spika. Unajua kwamba kama Waheshimiwa wamesimama na msimamo wao sioni ni sababu gani tunaweza hata kutupiana lugha ambayo haifurahishi wengine. Msimamo wako ni wako na hakuna mtu atakukataza. Hapa tuliuleta mswada wa kumng'atua Gavana akiwa ameketi hapa kwenye hiki kiti. Kama mtu ako na msimamo wake, tafadhali tuheshimiane. Hakuna mtu atakataza mwingine amtoe mwingine hapa. Tuwache lugha mbaya na kuwalaumu wengine kwa sababu hatuwezi kwenda njia moja sote. Mimi siko na nyinyi na ni vyema kusema ukweli….

Deputy Speaker: Order, Hon Jacob! Hon. Members, I really do not know that until we see a person being kicked out of this House that is the time you will understand what I am saying. I am simply saying that all people are respected here. Take your time, listen to another Member and he will also listen to you and then we will get a way forward.

Hon. Jacob Endom: Asante, Bwana Spika. Mimi huwa na msimamo na leo asubuhi nimekuja kwa ajili ya huo mswada kama niliye kwenye HBC. Nilisema wacha huu mswada uje utatue ile utatatua kwa sababu sio mama ama dada yangu mnamtoa. Mnasikia? Nilikutana nanyi hapa Bungeni na hatukuwa tunajuana. Ni Mungu alituleta tukakutana hapa. Nani alikuwa ananijua? Nimetoka huko msituni na tulikutana hapa na lazima tuheshimiane.

Kama tunaheshimiwa kila kitu kinaenda sawa kwa sababu wacha nikwambie, leo ni wewe kesho ni mwingine. Hii dunia tunaenda hivyo kwa hivyo ningemwambia Mheshimiwa Spika kwa sababu unaona vile hali ya nyumba iko lazima utoe njia ya kuendelea. Kama huo mswada hauko kwenye orodha umeona vile inaendelea kwa hivyo ni vizuri watu wakubaliane kitu kingine na wafanye.

Nilikuwa baraza la mji na Mheshimiwa Wachuka. Tulikuwa tukimtoa mwenyekiti vikundi vinagawanyika. Wengine wanaenda Meru wanafanya maneno yao na wengine wanaenda Nairobi. Siku ya mswada kwa meza vikundi vinapatana na mnachagua yule ntu mnataka. Ni haki yenu kumchagua yule mtu mnayemtaka kama viongozi wa hapa. Yule mtu hatatolewa hapa ni mimi kwa sababu nimechaguliwa Sosian na kuletwa hapa. Hivyo viti vingine vikikaa nitabaki Mjumbe wa Sosian kwa hivyo hakuna haja tupigane. Kama uko kwa kambi ile uko hakuna haja tupigane. Tuheshimiane tuone ya kwamba tumefanya ile kazi tutafanya.

Unajua kama kuna kitu kizuri mfanye ule mswada utakuja hapa ufurahisha kila mtu na mfanye kwa ile njia ya heshima. Unajiheshimu na ukifanya hivyo hata ukijificha wapi huo mswada utakuja hapa kwenye hii meza na utapita ama uanguke. Kitu cha maana ninawaomba waheshimiwa tafadhali mtulie muangalie njia ya kuendelea. Mfuate ile taratibu nilisema na nilikuwa peke yangu. Siwezikuwa HBC peke yangu na niwapitishie. Ni ukweli, basi ndugu zangu hatujakataa mswada wenu kuja hapa. Kila mtu ako na haki ya kuandika mswada uje hapa Bungeni kwa sababu mumechaguliwa na wananchi wa Laikipia. Hata Spika yuko na haki ya kuandikiwa mswada na kutolewa katika Bunge hili...

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Deputy Speaker: What is it Hon Zamzam?

Hon. Salma Zamzam: Bwana Spika, ningependa kumwarifu ndugu yangu tuliweza kutumia…

Deputy Speaker: Hon. Jacob, do you need some information?

Hon. Jacob Endom: No.

Hon. Salma Zamzam: Ni kumwarifu kwa sababu tuliweza kutumia sheria na HBC ilikataa kuketi…

Hon. Jacob Endom: Mheshimiwa, lazima uniheshimu kwa sababu mimi ndiye nimesimama hapa. Sikiza kile ambacho nasema kwa sababu nilikuheshimu mpaka ukamaliza. Bwana Spika, niko tayari kama imeletwa na nimeacha kazi zangu kwa sababu siku ya Alhamisi huwa naenda biashara zangu lakini nimekuja huku kwa sababu yenu. Lazima na nyinyi mheshimike na tafadhali mtulie kwa sababu huu mjadala utakuja. Hata kama itakuja Jumanne kaa na msimamo wako itakuja. Hakuna mtu atabadilisha. Nitafikisha hapo kwa sababu naona mwenzangu ana joto sana…

Deputy Speaker: What is it Hon. Zamzam?

Hon. Salma Zamzam: On a point of clarification Mr. Speaker. Hatuitaki Jumanne ila tunaomba leo huo mjadala ukuje. Tulisema huo mjadala ukuje leo lakini HBC hawakuketi. Walitugandamiza ili huu mjadala usipite katika Bunge hili. Mimi kama mfugaji narudia mjadala ukuje leo. Uajiri usimamishwe ili tuendelee na kazi. Jana tulisimamisha Bunge ili tuletewe mjadala leo lakini wametugandamiza na wamekataa kusikia kilio chetu kwa sababu sisi ni wanyonge. Katika HBC, Mheshimiwa Jacob peke yake ndiye amekuja. Hao wengine wako wapi. Saa hii tunafaa kuahirisha Bunge twende Nje ndio tuirudishe katika Bunge ama tuvunje kamati hiyo. Asante, Mheshimiwa Spika.

Hon. George Meshami: Asante sana, Mheshimiwa Spika. Jana tulikuwa na huu mjadala asubuhi na tukaahirisha Bunge ili tuwe na mjadala jioni. Tuliahirisha biashara za Bunge ndiyo leo asubuhi kuwe na biashara ambayo inafaa kuendelea. Hiyo biashara imesimama kwa sababu Mheshimiwa Spika umeshindwa. Bwana Spika, ulituambia jana kwa heshima la Bunge lako na Bunge ilikusikiza. Ulitoa mwongozo kwamba kufikia leo asubuhi mjadala uwe katika Bunge hili. Pia ulituambia utapigia Kamati ya Biashara za Bunge ili wapitishe huo mjadala.

Waheshimiwa walikwambia na pia wakapatana na Naibu Karani. Kilio cha Laikipia nzima kimekosa kusikizwa. Bwana Spika, ukiwa katika kiti chako tukufu ni kipi kingine unataka Bunge ifanye ilhali wamesema hakuna biashara itaendelea. Bwana Spika, umekosa mwelekeo na Bunge pia imeshindwa. Naomba Bunge iahirishwe tuingie katika majadiliano tena kwa sababu tumepoteza siku mbili muhimu ambazo tungezungumzia maendeleo ya wanalaikipia.

Naomba Bunge isimamishwe dakika thelathini tungoje Biashara ya Bunge ambayo wewe mwenyewe ulikiri ikuje katika Bunge. Kila mjumbe yuko na haki ya kuleta mswada ambao yeye mwenyewe anataka. Jana tulisema uajiri ambao umefanyika katika Bunge la

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Laikipia usimamishwe. Kwani kuna siasa zipi ambazo zinaendelea. Sisi ndio wenye kutunga sheria na tumechaguliwa kuwakilisha watu 500,000. Naomba mjadala ambao tulisikizana uje katika Bunge lako tukufu.

Hon. Irene Wachuka: Asante sana, Bwana Spika. Sisi hatutashinda hapa. Tunaomba dakika thelathini twende kisha tunaporudi tupate mjadala ukiwa hapa. Kama siyo hivyo hakuna kurudi nyuma ila tutafunga maofisi ya Karani na Spika watoke nje. Tutafunga saa hii. Sisi hatutakaa hapa tukingoja watu ilhali umekalia kiti. Hiyo ofisi haina watu lakini wako karibu. Sisi hatukulala tukipigiwa simu tukuje. Sisi hatutaki pesa ila tumekuja hapa kutetea Wanjiku. Hatutaki pesa ila tunataka kilio cha Wanjiku kisikike.

Kama siyo hivyo Karani na Spika watoke tufunge ofisi. Kama huo mjadala hautakuwa hapa wachukue makaratasi zao tuletewe mjadala wetu.

Hon. Catherine Kibue: Asante sana, Bwana Spika kwa kunipatia hii nafasi. Sina mengi ila nasimama kuungamana na wenzangu. Bwana Spika, mmetuangusha kwa uongozi. Mswahili alinena na kusema; '*heshima sio utumwa'*. Tunaomba Waheshimiwa wapatiwe haki yao. *'Mgalla muue na haki mpe'*. Hata kama mmetudharau kiasi kipi tunahitaji haki yetu. Hata kama mmeambia HBC waende na wazime simu mjadala uje Jumapili ili muwe mmefanya *lobbying*.

Hatuhitaji elfu hamsini zenu na kama hakuna mjadala katika Bunge tutafunga hizo ofisi zote kwa sababu hatuoni haja ofisi zikiwa zimefunguliwa ilhali wafanyikazi wanalipwa lakini hawapatii waheshimiwa haki yao. Bwana Spika, kwa heshima yote ukiwa Mheshimiwa kutoka Mashariki mwa Mukogodo tunakuheshimu na tunakupenda kwa hivyo uwache kutumika katika hili Bunge. Kwa hayo machache asante Bwana Spika na Mungu akubariki.

Hon. Simon Kanyutu: Thank you, Mr. Speaker. It is very unfortunate we are in the floor of this House deliberating issues that have been raised more than five times prior that ought to have been resolved by then before we come in the floor of this House. It is unfortunate a Whole House deliberating then agreeing on what is supposed to be done. It seems the leadership is not ready to give directions. We are in the floor of this House when the Mace is being guarded for Members being seen to be unruly.

Mr. Speaker, you need to give direction and we need to see the way forward because this is not the way to go. Mr. Speaker, we have essential matters that we ought to have deliberated today. I had a report that I was supposed to table in the floor of this House but nothing can proceed due to what is prevailing. Mr. Speaker, you need to give direction and we need to see this House in order. This is a House of Order but what is transpiring now seems that we are heading to a confrontation arena. That should not be the way for us to take.

Mr. Speaker, being on that Chair you need to give directions. We better adjourn this House rather than having an issue of moving all round for three sessions. Why don't we have a resolution to this we sort out rather than moving up and down? Mr. Speaker, anything can be resolved. There seems there are people who are aware of what is going on while others are not aware. Let it be open that this Assembly represents our people. We need everything to remain

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

open. If there is something we do not know we should be informed. Everything we need to know should be brought in the floor of the House. Mr. Speaker, we need your directions.

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

CANCELATION OF BBI MEETING

Deputy Speaker: Thank you, Hon. Members. First I would like to make some communication. Today we were travelling to Nairobi but unfortunately that meeting has been cancelled. I know some have seen in the media but it is good I do a communication. We are not going for that Bomas meeting.

Hon. Members, yesterday by reading the mood of the House some Members came to me and they had a motion they wanted to bring. Fortunately yesterday they drafted it at very late hours. Hon. Stephen, do you want to speak on my behalf…

Hon. Stephen Ndiritu: Yes I can Mr. Speaker. Mheshimiwa Spika, tulikuwa na wewe na huo mjadala tuliandaa saa kumi na moja jioni. Itakuwa ni aibu kuja katika Bunge hili kusema uongo. Huu ni mjadala ambao uko mbele ya vyombo vya habari na uliiona. Kuja hapa kutuambia mjadala uliandaliwa usiku. Mheshimiwa Spika, kama umeshindwa na kazi ondoka na usitutumie. Kama unatumiwa kutugandamiza sisi hatutakubali. Sisi tunataka demokrasia. Werevu ukikosa tutatumia ujinga.

Mheshimiwa Spika, usitumiwe kutukandamiza. Kama umeshindwa na kazi ondoka tuendelee. Tuko na Wabunge ambao wanaweza hiyo kazi. Uliambiwa hapa kuwa tunataka huu mjadala utengenezwe. Ukatuambia lazima kisha tukakuambia utoe amri ukapotea. Kupitia ujanja wetu na ujuzi tulio nayo tuko na mjadala hapo ambao umepokewa na Naibu Karani. Bwana Spika usipotoshe Bunge hili. We cannot allow you to dictate this Assembly the way the Clerk is doing. Thank you.

Deputy Speaker: Thank you, Hon. Stephen. I said that we left late and this motion was drafted late. I received the motion that was drafted. My duty was to call for a HBC meeting which I did. This morning we were unable to reach the HBC quorum. That was one of the reasons that made the motion not to come to the floor of this House. Hon. Members, we made a step from where we were yesterday because where we were the motion was not drafted. I said we will push it until it is drafted.

I never knew that I will push Hon. Members to get to HBC meeting. Once they received the invitation letter a quorum did not turn up. As I said yesterday people have their rights to be heard including bring motions. Nobody will intimidate anyone in the angle…

Hon. Chris allow me to finish so that I give you time. So that we do not try to block some people. We will give you enough time but Hon. Members as I said yesterday let us use the right procedure. Anyone can challenge you if you are not trying to use the right procedure. We still have the HBC meeting like any other time but for today it has not reached quorum. I will ask why the motion has not come in the floor of this House. I would like to confirm in this House that that motion is already on the table and we are working on it. In the near future we shall bring it in the floor of this House…

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Chris if you keep on disturbing us you are not respecting the Chair. I kept on saying that every person will be given time to talk. Why don't you…

Hon. Chris Mark: Mr. Speaker, I have respected you and that is why I have not yelled. I just raised my microphone but you are assuming me. As much as that chair must be blind, when you come and talk issues of you want the motion to come here, that is not your job. You are not the legal person here Mr. Speaker. I don't know why you are interfering with this process. This is not a lie at night you were very uncomfortable. You even called many people asking what you will do with that thing.

That seat requires a lot of wisdom and I will tell you we respect you as a Hon. Member of Mukogodo East and even more because you sit on that chair. Do not think that that Chair has immunity. You are not going to tell us a lot of stories. We had two Hon. Members of the House Business Committee this morning. Some just walked and said they cannot be part of this and this is simple that this business of this House is not going to continue.

Do not think you are going to the next order because this is abuse of office. The Committee of the House Business is not doing us any favour. In fact, it is us doing them favour because we approved them in this House. Let them never think they are doing us favour. Do not start saying that the motion was given out at night. Those are stories and I remind you there is a reason we might not be the brightest here. We may not have stayed in politics the longest but we are not stupid when we told you to give a direction which you refused. Maybe you have a master who you are answerable to.

Phone calls were made at night and some in the morning and recordings are there. I said earlier on that Hon. Members are very rich in this Assembly of Laikipia. God has really blessed them. Kshs. 50,000 or 100,000 cannot work. 200,000 not even a budget for a day. Kshs. 500,000 is not a budget for a week and Kshs.1 million is not a budget for a month. In fact, the salaries you pay us is gratuity but we do not survive on that. We are doing this not as a job but as a calling.

Do not sit there as leadership thinking that you are doing this because we want that money so much. You people told us the amount and we are going to hold you accountable. We do not want stories of the business of the House. Adjourn for one hour so that those in HBC be called and if they cannot make it in one hour let us come back and see. Mr. Speaker, do not speak on their behalf. Let us go outside for one hour. Let them be called one by one starting with the leader of government business of the House who is the Majority Leader.

We are going to be in Laikipia today until that motion comes here. Do not take us around because we have been patient and diplomatic but do not take us for weakness Mr. Speaker.

Hon. Salma Zamzam: Asante sana, Mheshimiwa Spika. Nimesikia ukichangia mswada wako na kutuambia huu mjadala uko na changamoto nyingi. Mjadala wa kuondoa Waziri wa Fedha haukuwa na changamoto ni kumaanisha kuondoa Karani wa Bunge itakuwa na changamoto. Bwana Spika, umetuambia Kamati ya Biashara katika Bunge wamefika kisha wakatoka na kuenda zao. Hili Bunge halina wajumbe wote ila kuna wajumbe ambao hatuko

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

nao. Wamejieleza hapa kwa kumbukumbu ya Bunge hawako kwa sababu maslahi yao ya kibinafsi iliangaliwa.

Siongopi kusema na nitarudia kwamba maslahi yao ya kibinafsi yaliangaliwa. Mnangoja ifike Jumanne ili mshawishi waheshimiwa wengine. Sisi wenye hatuko na wao tunalilia haki ya wanyonge wa Laikipia ambao wamegandamizwa. Bwana Spika, msikuje kutapitia maneno ilhali tumekupatia kiti cha Spika kama mwakilishi wa wodi ilhali tunashangaa Spika ambaye tulimchagua yuko wapi. Bwana Spika, unaogopa kupatiana mwongozo wako. Sisi hatuna mengi tunataka tu uajiri wa watu usimamishwe urudiwe upya. Hatuna vita na mtu.

Usiogope kutuambia iko na changamoto kwa sababu hapa hakuna wakili. Tunataka kusikia wakili ambaye amesema iko na changamoto atuambie ni zipi ambazo hatujui. Wakati tunaandika mjadala tunajua ni kwa nini tunaandaa ndiyo iletwe katika Bunge hili. Tunaomba Bunge iahirishwe kwa saa moja ama mbili ili tuweze kuelewana ili turudi na muswada wetu ambao tutapitisha. Hatuendi mpaka tuone muswada. Tunakwambia hivyo ujue na mkikataa tutaigiza hapa leo.

Kama hatutumii akili wacha tuitwe wajinga leo. Tuache kudanganyana na kucheza. Hakuna waheshimiwa wakubwa kuliko wengine. *Adjourn the sitting*. Kuna waheshimiwa hapa wanapiga simu wakiitwa kwa sababu tunagonga serikali. Hatugongi serikali ila tulisema uajiri katika Bunge la Laikipia usimamishwe ilhali uliendelea. Hicho ndicho kilio chetu. Kama mtatuweka mpaka Jumanne ili tupatane na wanaume wengine watapata. Tunasikia wanatafuta nambari. Sisi ni Serikali ambayo inatetea BBI ambayo ni hili Bunge. Sisi ndio tunasimamia serikali. Kiongozi wa Walio Wengi yuko wapi. Tunamtaka Mheshimiwa Thomi katika Bunge hili. Hakuna haja ya kuongea uongo. Uongozi wa Bunge hili umetuangusha na tutamalizia hapo. Tunafunga Bunge Bwana Spika, Asante sana.

ADJOURNMENT

Deputy Speaker: Hon. Members, the sittings of this House stands adjourned until Tuesday 17th November, 2020 at 2.30 p.m.

The House rose at 10.13 a.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*